www.tea.or.tz

# MFUKO WA ELIMU

## TEA KUTUMIA SH. BIL. 3.0 KUBORESHA UTEKELEZAJI WA MTAALA MPYA WA ELIMU NCHINI



Toleo la 5
Oktoba - Disemba
2024

>> MAFUNZO YA UJUZI YANAVYOBADILI MAISHA YA AKINA MAMA.

>> WANAFUNZI WA TABORA BOYS WAPONGEZA UKARABATI WA TEA.

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*

# KUHUSU TEA

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)** ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

**Mfuko wa Elimu**

Mfuko wa Elimu unapokea rasilimali fedha na vifaa ambazo hukusanywa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tazania (TEA) kwa lengo la kufadhili miradi ya elimu nchini kutoka vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

TEA imepewa jukumu la kuhamasisha wadau mbalimbali nchini na nchi za nje kuchangia raslimali mbali mbali kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali kuinua ubora, na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa



## DIRA

Kuwa Mfuko wa Elimu bora wenye hadhi ya kimataifa unao tatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



## DHAMIRA

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

# YALIYOMO

Salaam za Mkurugenzi Mkuu....................................................ii

TEA Kutumia Sh. Bilioni 3.0 Kutumika Kuboresha Utekelezaji wa Mtaala mpya wa Elimu Nchini..........................................01

Maabara za Sayansi Zaongeza Hamasa ya Masomo Kakonko Girls........................................................................02

TotalEnergies Yasaidia Kuimarisha Elimu na Ustawi wa mtoto wa kike........................................................................03

Wanafunzi wa Tabora Boys Wapongeza Ukarabati wa TEA, Wataka vifaa vya Tehama ....................................................04

Habari Katika Picha: Hafla ya Kukabidhi Msaada wa Taulo za kike..................................................................................05

Mafunzo ya Ujuzi Yanavyo Badili Maisha ya Akina Mama Tabora..................................................................................07

Wanafunzi 400 Kunufaika na Shule Mpya Kijiji cha Songambele- Kibondo...........................................................09

Milioni 52.2 Zagharamia Ukarabati wa Madarasa Shule ya Msingi Lwasho - Momba.......................................................10

# TIMU YA UHARIRI

**Mwenyekiti:** Masozi Nyirenda

**Mhariri:** Bestina Magutu

**Wachangiaji:** Eliafile Solla

Joyce Minja

# ANUANI:

**Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)**

**S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania**

**Barua pepe: info@tea.or.tz,**

**Tovuti www.tea.or.tz,**

**Instagram: Officialteatz,**



## SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU

Karibu kwenye toleo hili la tano la Jarida la Mfuko wa Elimu, linaloangazia juhudi mbalimbali za kuboresha sekta ya elimu nchini. Katika kipindi hiki, TEA imeendelea kutekeleza miradi muhimu inayolenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Katika toleo hili, tunawaletea taarifa kuhusu uwekezaji wa Shilingi Bilioni 3.0 kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu nchini. Shule 20 kutoka mikoa 15 zitafaidika na ufadhili huu, utakaosaidia kuimarisha miundombinu ya elimu, ikiwemo vyumba vya madarasa, viwanja vya michezo, karakana na vifaa vya TEHAMA.

Pia, tunamulika mradi wa ujenzi wa maabara za sayansi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko, Kigoma, ambazo zimeongeza hamasa kwa wanafunzi wa sayansi. Katika sekta ya ustawi wa watoto wa kike, kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, kwa kushirikiana na TEA, imetoa msaada wa taulo za kike kwa shule za sekondari, hatua inayolenga kuboresha mahudhurio ya wanafunzi wa kike na kuwapa fursa sawa kielimu.

Katika jitihada za kuboresha mazingira ya kujifunzia, wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Tabora Boys wamepongeza TEA kwa ukarabati wa miundombinu ya shule yao, huku wakielezea hitaji la vifaa zaidi vya TEHAMA ili kuboresha ujifunzaji wa masomo ya sayansi na teknolojia.

Aidha, tunakuletea simulizi za mafanikio ya mafunzo ya ujuzi yanayofadhiliwa na TEA kupitia SDF, yanayobadilisha maisha ya wanawake nchini. Tukiangalia simulizi za wanufaika kama Ashura Mwazembe wa Tabora, ambaye sasa anaendesha biashara ya usindikaji wa chakula na kusaidia vijana kujifunza ujuzi wa kujiajiri.

Jarida hili linahakikisha kuwa unapata taarifa sahihi na za kina kuhusu maendeleo ya sekta ya elimu nchini kupitia miradi ya TEA. Tunaendelea kushirikiana na wadau wa elimu, sekta binafsi, na mashirika ya kimataifa ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu bora na mazingira mazuri ya kujifunzia.

**Dkt. Erasmus F. Kipesha**
*Mkurugenzi Mkuu-TEA*

# TEA KUTUMIA SH. BILIONI 3.0 KUBORESHA UTEKELEZAJI WA MTAALA MPYA WA ELIMU NCHINI

Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) umepanga kutumia **Sh. bilioni 3.0** katika miradi ya kuboresha mazingira ya utekelezaji wa mtaala mpya wa masomo ulioanza kutumika Januari 2025.

Shule 20 kutoka mikoa 15 zitanufaika na ufadhili huo.Shule hizo ni Sekondari za Usangi (Kilimanjaro), Arusha (Arusha), Dar es Salaam (Dar es Salaam), Matola (Njombe), Nkowe (Lindi), Ukombozi (Urambo - Tabora), Morogoro (Morogoro), Chang'ombe (Dar es Salaam), Chie Serwaat (Mbulu - Manyara), na Kigoma (Kigoma).

Shule nyingine ni Sekondari za Mbeya (Mbeya), Darajani (Dodoma), Pamba (Mwanza), Iyunga (Mbeya), Uwemba (Njombe), Mafiga (Morogoro), Msangano (Momba - Songwe), Sekondari ya Wasichana Iringa (Iringa), Sekondari ya Wasichana Korogwe (Tanga), na Sekondari ya Wavulana Bwiru (Mwanza).

Fedha hizo zitatumika kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo ya ubunifu na ushonaji wa nguo, michezo, upishi, kilimo, sanaa za majukwaa, pamoja na mafunzo mengine ya ufundi na ufundi stadi.

Miradi mingine itakayofadhiliwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 ni pamoja na:

- Ujenzi wa vyumba **56** vya madarasa kwa **Sh. Bilioni 1.2**
- Ujenzi wa matundu **336** ya vyoo kwa **Sh. Bilioni 7.1**
- Ujenzi wa nyumba **12** za walimu 12 kwa **Sh. Milioni 605**
- Ujenzi wa mabweni **08** kwa **Sh. Bilioni 1.1**
- Ujenzi wa maabara **12** za sayansi kwa **Sh. milioni 472.4**
- Umaliziaji wa miundombinu katika shule **39** kwa **Sh. Bilioni 1.2**
- Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa shule **tisa (09)** kwa gharama ya **Sh. milioni 544**

Katika utekelezaji wa majukumu yake kama taasisi ya Muungano, TEA imetenga **Sh. milioni 320.9** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maktaba kubwa ya Taasisi ya Huduma za Maktaba ya Zanzibar (ZLSB), itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia watu takriban 1,500 kwa wakati mmoja.

Kwa ujumla, **Sh. Bilioni 11.3**. zitatumika kutekeleza miradi ipatayo **113,** ambayo itanufaisha wanafunzi **29,482** na walimu **12** pamoja na familia zao katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaini bango lenye ujumbe kuhusu elimu wakati wa hafla ya uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 katika viwanja vya ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma*

# MAABARA ZA SAYANSI ZAONGEZA HAMASA YA MASOMO – KAKONKO GIRLS

Ujenzi wa maabara tatu za Sayansi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko, Kigoma, umeleta hamasa kubwa ya kitaaluma kutokana na kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Maabara hizo za Fizikia, Kemia, na Biolojia, zilizogharimu shilingi milioni 180, zilijengwa kwa ufadhili wa Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu wa Taifa (TEA). Shule hii yenye wanafunzi 270 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne imepata mwamko mpya wa elimu, jambo lililowaletea furaha walimu na wanafunzi.

Mkuu wa shule hiyo, Antoria Paul Nkabo, alisema kukamilika kwa mradi huu kutaongeza hamasa ya wanafunzi kufanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi kutokana na mazingira bora na rafiki ya kujifunzia kwa vitendo. “Kwa kupata mradi huu, tunakwenda kuongeza ufaulu. Tunatarajia nusu ya wanafunzi (167) watakaoingia kidato cha nne wapate daraja la kwanza katika mitihani yao ya mwisho,” alisema.

Mwalimu wa Kemia na Biolojia, Nikolous Kayombo, aliongeza kuwa awali walifundisha masomo hayo kwa nadharia pekee, lakini sasa, kupitia maabara hizi, wanafunzi wataweza kujifunza kwa vitendo, hivyo kuongeza uelewa na ufaulu wao.

Wanafunzi Zulfa Twaha, Happines Amosi na Sharifat Hamad walitoa shukrani zao kwa UNICEF na TEA kwa kuwapatia maabara hizi muhimu. Walibainisha kuwa maabara hizi zinawawezesha kufanya majaribio mengi ya masomo ya sayansi, jambo linalochochea mafanikio yao kitaaluma.

Mbali na maabara, TEA pia ilitoa ufadhili wa ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 mwaka 2022/2023, kwa gharama ya zaidi ya Sh. mil. 142.9.

Mwanafunzi Sharifat alieleza kuwa bweni hilo limeboresha makazi yao, hivyo kuwawezesha kujikita zaidi katika masomo.

Shule ya Wasichana Kakonko iliyoanzishwa mwaka 2022 ina jumla ya wanafunzi 274, na mwaka 2025 inatarajia kudahili wanafunzi wengine 100 wa kidato cha kwanza, jambo linaloashiria maendeleo endelevu shuleni hapo.

Awali katika ziara yake katika mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Kakonko Kanali Evance Mlassa, amepongeza TEA na UNICEF kwa kufanikisha ufadhili wa ujenzi wa maabara hizo na kusisitiza utunzwaji ili kudumu na kuwanufaisha wanafunzi wengi Zaidi.

Mbali na Mradi wa maabara za sayansi Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepata ufadhili mwingine wa UNICEF Tanzania wa ujenzi wa matundu 12 ya choo katika shule ya msingi Kagondo kwa thamani ya Sh milioni 59.4

Miradi hii ni sehemu ya miradi 13 iliyofadhiliwa na UNICEF kwa kushirikiana na TEA katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, ikiwa na thamani ya jumla ya Shilingi milioni 834. Miradi hiyo imehusisha ujenzi wa maabara, matundu ya vyoo, na vyumba vya madarasa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, na Songwe.

Ushirikiano kati ya TEA na UNICEF unaendelea kuwa mfano bora wa juhudi za pamoja katika kuinua viwango vya elimu kwa walimu na wanafunzi nchini Tanzania. Walimu wanawezeshwa kufundisha kwa weledi zaidi, na wanafunzi wanapata elimu bora ambayo inawaandaa kwa changamoto za siku zijazo.



*Maafisa kutoka UNICEF Tanzania na TEA wakiangalia vifaa katika maabara ya Fizikia katika shule ya sekondari ya wasichana Kakonko.*

# TOTALENERGIES YASAIDIA KUIMARISHA ELIMU NA USTAWI WA MTOTO WA KIKE

Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), imekabidhi katoni 360 za taulo za kike zenye thamani ya Shilingi milioni 25.5 kwa shule nne za sekondari tarehe 22 Novemba 2024. Shule zilizonufaika ni Sekondari ya Lemira (Hai, Kilimanjaro), Sekondari ya Sitalike (Katavi), Sekondari ya Mkombozi (Same, Kilimanjaro), na Sekondari ya Isack Kamwelwe (Katavi). Msaada huu unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wanafunzi 1,200 kwa mwaka mzima.

Msaada huu wa taulo za kike utasaidia kuboresha mahudhurio na utendaji wa wanafunzi wa kike kwa kuongeza mahudhurio ya wanafunzi wa kike, hasa wakati wa siku za hedhi, na kuondoa changamoto za kijamii zinazosababisha kukatisha masomo. Hali hii itasaidia kuongeza ushindani wa kitaaluma na ufaulu wa masomo yao.

Mwalimu Glory Michael wa Sekondari Mkombozi alisema: "Msaada huu unaweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wa kike kufanikisha masomo yao kwa utulivu, hali ambayo inachochea usawa wa kijinsia darasani."

Bw. Philipo Silvester Mwalimu Mkuu kutoka Shule ya Sekondari Lemira alisisitiza kuwa unapomuinua mtoto wa kike umeinua taifa hivyo kupongeza TEA na Totalenergies Marketing Tanzania Ltd kwa kuwezesha msaaa huo wa taulo za kike.

Kampuni ya Totalenergies Marketing Tanzania Ltd pia katika mwaka 2024 imetoa msaada wa madawati 200 kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa yaliyotolewa mwaka huu kwa shule tatu mkoani Pwani na Dar es Salaam hivyo kuongeza nafasi za kukaa kwa wanafunzi na kuboresha hali ya kujifunzia.

Kaimu Mkurugenzi wa TEA, Bw. Masozi Nyirenda, ameipongeza TotalEnergies kwa kuchangia juhudi za serikali katika kuboresha sekta ya elimu, akisisitiza kuwa msaada huu ni mfano bora wa ushirikiano wa sekta binafsi na umma.

Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa TotalEnergies, Bi. Getrude Mpangile, ameahidi kuwa kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na TEA na taasisi nyingine kuboresha sekta ya elimu, hasa kwa watoto wa kike.




*Walimu kutoka shule zilizonufaika na msaada wa taulo za kike katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa TotalEnergies, Bi. Getrude Mpangile (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji wa Raslimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu wa TEA, Bw. Masozi Nyirenda (kulia).*

# WANAFUNZI WA TABORA BOYS WAPONGEZA UKARABATI WA TEA, WATAKA VIFAA VYA TEHAMA

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora , mkoani Tabora, wamepongeza ukarabati wa miundombinu shuleni mwao uliotekelezwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa (TEA). Ukarabati huo umeboresha mazingira ya kujifunzia na kutajwa kama hatua muhimu kwa ustawi wa jumuiya ya shule hiyo.



*Wanafunzi wakipata maelezo kuhusu majukumu ya Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA katika maonyesho yaliyofanyika viwanja vya Chipukizi, Tabora.*

Wakizungumza katika Maonyesho ya Maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima (Oktoba 7-11, 2024) yaliyofanyika viwanja vya Chipukizi, wanafunzi walieleza kuwa kabla ya ukarabati, mabweni na miundombinu mingine yalikuwa katika hali duni.

Zalius, mwanafunzi wa kidato cha sita, alikumbuka hali mbaya ya shule wakati alipojiunga kwa masomo ya O-level, akisema kuwa ukarabati huo umewanufaisha sana wanafunzi kwa kuboresha mazingira yao ya kujifunzia.

Hata hivyo, wanafunzi walibainisha changamoto zinazobaki, hususan uhaba wa kompyuta na upatikanaji wa mtandao wa intaneti.

Zalius alieleza kwamba kutokana na uhaba wa vifaa, wanafunzi wa vidato vya juu, hasa kidato cha nne hadi cha sita, hupata nafasi ya kutumia chumba cha kompyuta kwa zamu, jambo linalopunguza ufanisi wa mafunzo yao.

Pia, waliomba vifaa zaidi vya TEHAMA kwa maelezo kuwa vitawasaidia wanafunzi wa mkondo wa PCM (Fizikia, Kemia, na Hisabati).

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilikuwa miongoni mwa taasisi zilizoshiriki maadhimisho hayo na kuelezea jitihada zake za kuboresha mazingira ya elimu kwa ufadhili na miradi mbalimbali inayowezesha maendeleo ya shule nchini.

# HABARI KATIKA PICHA: HAFLA YA KUKABIDHI MSAADA WA TAULO ZA KIKE




*Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu wa TEA, Bwana Masozi Nyirenda (Kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano ya Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Bi Getrude Mpangile katika halfa ya kukabidhi msaada wa taulo za kike katoni 360 Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd na wawakilishi wa shule za Sekondari ya Lemira (Hai, Kilimanjaro), Sekondari ya Sitalike (Katavi), Sekondari ya Mkombozi (Same, Kilimanjaro), na Sekondari ya Isack Kamwelwe (Katavi) katika picha ya pamoja.*

# HABARI KATIKA PICHA: HAFLA YA KUKABIDHI MSAADA WA TAULO ZA KIKE




*Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Isack Kamwelwe Bi. Debora Conrad Nguvumali (Kati) katika kicha ya pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimizi wa Miradi ya Elimu wa TEA, Bwana Masozi Nyirenda (Kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano ya Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Bi Getrude Mpangile katika halfa ya kukabidhi msaada wa taulo za kike katoni 360 Jijini Dodoma.*




*Bw. Philipo Silvester Mwalimu Mkuu kutoka Shule ya Sekondari Lemira. (Kati) katika kicha ya pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu wa TEA, Bwana Masozi Nyirenda (Kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano ya Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Bi Getrude Mpangile katika halfa ya kukabidhi msaada wa taulo za kike katoni 360 Jijini Dodoma.*




*Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu wa TEA, Bwana Masozi Nyirenda (Kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano ya Kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Bi Getrude Mpangile katika picha ya pamoja na walimu wa shule zilizonufaika na msaada wa taulo za kike katoni 360 Jijini Dodoma.*

# MAFUNZO YA UJUZI YANAVYOBADILI MAISHA YA AKINA MAMA - TABORA (Inaendelea uk. wa 07)




*Bi. Ashura Mwazembe kutoka kikundi cha Asili Nuru Honey and Food Processors akizungumza na wadau katika viwanja vya Chipukizi, Tabora.*

Ashura Mwazembe, kutoka kikundi cha Asili Nuru Honey and Food Processors, anaonyesha furaha na shauku anapozungumzia mafunzo ya usindikaji wa chakula aliyopokea kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) kwa ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Bi. Mwazembe, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wajasiriamali wa Mkoa wa Tabora, anasema mafunzo hayo yaliyoendeshwa na SIDO-Tabora kwa ushirikiano na Chuo cha Masuala ya Nyuki, yameleta mafanikio makubwa kwake.

“Sasa namiliki maduka mawili hapa Tabora ambapo nauza bidhaa zilizosindikwa, ikiwemo asali. Nimenunua mashamba ya nyuki, nimejenga nyumba, na sasa naweza kuhudumia familia yangu,” alisema Bi. Mwazembe, mmoja wa wanufaika zaidi ya 400 wa mafunzo hayo mwaka 2022.
Bidhaa za asali kutoka kikundi chake zimepata soko ndani na nje ya Tanzania, zikifika mpaka Rwanda na Burundi. Ameeleza kuwa serikali imekuwa ikiwawezesha kuhudhuria maonyesho maarufu ya wajasiriamali ya Juakali yanayowaleta pamoja wajasiriamali wa Afrika Mashariki. Kikundi chake kimehudhuria maonyesho nchini Tanzania, Burundi, na Rwanda.

Kama jitihada zake za kurejesha fadhila kwa jamii, Bi. Mwazembe anatoa mafunzo kwa vijana wa Tabora, akiwahamasisha kuanzisha miradi ya kujiajiri. “Nimefundisha wanafunzi wa Tabora Girls kutengeneza sabuni, na sasa wanafanya hivyo. Pia nimefundisha wanafunzi wa Chuo cha Nyuki Tabora na nimealikwa kutoa mafunzo katika mikoa mingine,” alisema.

Akionyesha tabasamu la furaha, Bi Mwazembe alisimulia jinsi ujuzi alioupata ulivyomsaidia kumfundisha binti mmoja kutoka familia yenye changamoto za kiuchumi. “Sasa binti huyo anasaidia familia yake kwa kipato alichopata kupitia ujuzi huo, hata kuwasomesha wadogo zake,” alisema.

# (Kutoka uk. wa 07) MAFUNZO YA UJUZI YANAVYOBADILI MAISHA YA AKINA MAMA - TABORA

Mwamvua Hisa Hamisi, kutoka Kaliua Mkoani Tabora, alipokea mafunzo ya usindikaji kupitia SDF mwaka 2019 na ameweza kufuga nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa.

Akiwa Mwenyekiti wa Wafugaji Nyuki Kaliua, Mwamvua alisema mafunzo hayo yaliboresha mbinu zake za kufungasha bidhaa, na hivyo kupanua soko lake ndani na nje ya nchi. Kikundi chake chenye wanachama 15 kimenufaika na mkopo wa Sh. milioni 10 kutoka halmashauri, na sasa kinaendesha duka la kuuza asali linaloingiza kipato cha kikundi.

Paulina Martina N'ghumbi, mstaafu wa utumishi wa umma kutoka Urambo, alitumia fursa ya mafunzo ya SDF kujihusisha na usindikaji wa mazao kama karanga na asali. Akiwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi Urambo, anahimiza watu kuchangamkia mafunzo.

Meneja wa SIDO Tabora alisema baada ya kutoa mafunzo, shirika lilinunua mashine za kuchujia asali ambazo zilikabidhiwa kwa halmashauri za mkoa. "Mashine hizi zimetolewa kwa Makatibu Tawala wa Wilaya na kuwekwa kwenye maeneo maalum ili kusaidia wazalishaji wadogo," alisema. Mashine hizo zimeongeza ubora wa asali na kuwasaidia wanufaika kufikia masoko ya kimataifa.

Kwa miaka mitano, TEA kupitia mradi wa SDF imewezesha mafunzo ya ujuzi kwa zaidi ya vijana na wanawake 44,000 nchini, ikibadilisha maisha na kuboresha fursa za kiuchumi.




*Bi. Mwamvua Hisa Hamisi, mmoja wa wanufaika wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi, akizungumza na wadau katika viwanja vya Chipukizi, Tabora.*

# WANAFUNZI 400 KUNUFAIKA NA SHULE MPYA KIJIJI CHA SONGAMBELE - KIBONDO

Watoto zaidi ya 400 kutoka kijiji cha Songambele kilichoko kata ya Kumsenga - Kibondo mkoani Kigoma wanatarajia kunufaika na huduma ya shule mpya shikizi kufuatia ufadhili wa Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu wa Taifa (TEA) unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Ufadhili huo umefanikisha ujenzi wa madarasa manne na ofisi moja ya walimu kwa gharama ya shilingi milioni 58. Mradi huu umekamilisha maboma ya madarasa na ofisi yaliyokuwa yameanzishwa na nguvu za wananchi. Shule hiyo shikizi inatarajiwa kuanza kutumika mapema mwaka 2025, ikiwahudumia wanafunzi wa masomo ya awali, darasa la kwanza hadi la tatu hivyo watoto wa kijiji cha Songambele hawatalazimika tena kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 3 kwenda na kurudi shuleni.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kibuye, Bw. Micheal Mgonja Mpuko, aliyeko kusimamia shule hiyo shikizi, amesema kuwa maboresho haya yatapunguza changamoto za wanafunzi wa eneo hilo kulazimika kutembea mwendo mrefu kila siku.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wazazi, Mch. Esron Marko Baseka, ameshukuru UNICEF na TEA kwa kufanikisha mradi huo na kuwataka wazazi wa kijiji cha Songambele kuwahamasisha watoto wao kwenda shule.



*Mradi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu kwa ajili ya shule shikizi katika kijiji cha Songambele, kata ya Kumsenga, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, Kigoma, uliofadhiliwa na UNICEF-Tanzania kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA.*

# MILIONI 54.2 ZAGHARIMIA UKARABATI WA MADARASA SHULE YA MSINGI LWASHO - MOMBA

Jumla ya Shilingi milioni 54.2 zimetumika kukarabati vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Msingi Lwasho, iliyopo Halmashauri ya Momba, Mkoa wa Songwe. Mradi huo umefadhiliwa na UNICEF kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Lengo kuu la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya elimu na kuweka mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia.Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lwasho, Bw. Godfrey Alban Mligo, amesema shule hiyo inayohudumia wanafunzi zaidi ya elfu moja, wakiwemo wanafunzi 200 wa shule shikizi, ilikabiliwa na changamoto ya uchakavu wa vyumba vya madarasa kabla ya mradi huu.

Bw. Mligo ameeleza kuwa ukarabati huu umeleta mabadiliko makubwa kwani sasa wanafunzi wanavutiwa zaidi kuhudhuria masomo kutokana na mazingira bora ya madarasa. Wanafunzi wa darasa la sita, Tecra Leonard Silungwe na Peter Elias Shija, wameeleza furaha yao kwa hatua hii, wakibainisha kuwa madarasa hayo sasa yana mwanga wa kutosha, sakafu isiyo na vumbi, na mazingira mazuri kwa ajili ya kujifunza. Mradi huu ni sehemu ya juhudi za TEA na UNICEF za kuhakikisha miundombinu ya elimu inaboreshwa ili kutoa fursa sawa za elimu kwa watoto nchini Tanzania.



*Bw. Godfrey Alban Mligo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lwasho, katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba, mkoani Songwe (watatu kutoka kushoto) akizungumzia mradi wa madarasa uliofadhiliwa na UNICEF-Tanzania kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA.*



*Mradi wa madarasa katika Shule ya Msingi Lwasho uliofadhiliwa na UNICEF-Tanzania kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA*

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**
**S.L.P. 2516, Dodoma Tanzania.**

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*